



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

**MWALIKO WA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO
LA SONGEA MJINI, SINGIDA KASKAZINI, LONGIDO NA UDIWANI KATIKA
KATA 5 KWENYE HALMASHAURI TANO (5) ZA TANZANIA BARA**

Kwa mujibu wa kifungu cha 46 (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Songea Mjini, Singida kaskazini, Longido na Udiwani katika Kata tano (5) kwenye Halmashauri Sita (6) za Tanzania Bara, kujaza nafasi wazi.

Kwa ajili ya kuweka uwazi katika Uchaguzi huo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia Kanuni ya 18 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge 2015, inapenda kualika Asasi za Kiraia na Taasisi mbalimbali za ndani zinazotaka kuwa Watazamaji wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mdogo unaotarajiwa kufanyika tarehe **13/01/2018**.

Majimbo yatakayofanya Uchaguzi Mdogo ni:-

Na.	Mkoa	Jimbo	Halmashauri
1	Ruvuma	Songea Mjini	Manispaa ya Songea
2	Singida	Singida Kaskazini	Singida DC
3	Arusha	Longido	Longido DC

Kata katika Halmashauri tano (5) za Tanzania Bara.

Na	Mkoa	Halmashauri	Kata
1	Kagera	Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.	Keza
2	Arusha	Halmashauri ya Jiji la Arusha	Kimandolu
3	Pwani	Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe	Kurui
4	Tabora	Halmashauri ya Wilaya ya Uyui	Bukumbi
5	Tanga	Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe	Kwagunda

Asasi/Taasisi zinapaswa kuzingatia masharti yafuatayo wakati wa kuwasilisha maombi yao:-

- (i) Anuani Kamili ya Taasisi husika,
- (ii) Anuani ya Makazi ya Ofisi ya Taasisi husika ilipo,
- (iii) Mahali /Sehemu ambapo Taasisi husika inafanya kazi.
- (iv) Shughuli ambazo zinafanywa na Taasisi husika kwa mujibu wa Hati ya Usajili
- (v) Kutaja sehemu ambazo Asasi/Taasisi inataka kufanya zoezi hilo la Utazamaji.
- (vi) Kutaja idadi ya watu ambao Taasisi / Asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao.
- (vii) Kutaja majina na namba za simu za viongozi wa Taasisi husika kama yalivyoandikwa katika Hati za Usajili wa Taasisi.
- (viii) Ikiwa Taasisi inahusisha Watendaji wa Kimataifa, wawili lazima wawe watanzania.
- (ix) Kuambatanisha nakala/kivuli cha hati ya Usajili wa Taasisi husika.
- (x) Kuambatanisha nakala / kivuli cha Katiba ya Taasisi / Asasi husika.

Vilevile, Taasisi zitakazopewa vibali vya kuwa Watazamaji zitapaswa kuzingatia Mwongozo kwa watazamaji wa ndani na wa Kimataifa ulioandaliwa na Tume kwa mujibu wa Kanuni ya 24 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge na Kanuni ya 20 ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2015

Maombi ya kuwa Watazamaji wa Uchaguzi yatapaswa kuwasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Makao Makuu kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Posta House, Ghorofa ya 7,
Mtaa wa Ghana/Ohio,
S. L. P. 10923,
DAR ES SALAAM.